JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA KILIMO



MWONGOZO WA UTATUZI WA

MIGOGORO KATIKA VYAMA VYA USHIRIKA

Imeandaliwa na:
Tume ya Maendeleo ya Ushirika,
S. L. P. 201,
DODOMA

TOLEO LA PILI JULAI, 2026


DIBAJI

Vyama vya Ushirika nchini vinachangia katika maendeleo ya jamii pale ambapo vinafanya kazi vizuri kwa kuzingatia sheria na taratibu zilizowekwa katika kuvisimamia. Hata hivyo, kumekuwa na changamoto katika baadhi ya Vyama vya Ushirika kutumia muda mrefu katika migogoro na kusababisha kurudisha nyuma maendeleo ya Vyama hivyo vya Ushirika.

Mrajis wa Vyama vya Ushirika ameandaa Mwongozo wa Utatuzi wa Migogoro katika Vyama vya Ushirika kwa lengo la kuweka utaratibu wa namna bora ya kutatua migogoro inayojitokeza katika Vyama vya Ushirika kwa kuzingatia Sheria ya Vyama vya Ushirika (Sura ya 211), Kanuni za Vyama vya Ushirika za mwaka 2015 na Sheria mbalimbali za nchi.

Aidha, Mwongozo huu utawasaidia wadau mbalimbali kuhakikisha kwamba utatuzi wa Migogoro yote katika Vyama vya Ushirika nchini unafanywa kwa kuzingatia Mwongozo huu na Sheria husika. Wadau hao ni pamoja na Tume ya Maendeleo ya Ushirika,Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Wizara za kisekta, wanachama, viongozi na watendaji wa Vyama vya Ushirika pamoja na Taasisi mbalimbali zinazofanya kazi na Vyama vya Ushirika.

Ni matarajio ya Mrajis wa Vyama vya Ushirika kuwa, Mwongozo huu utasaidia kutatua changamoto zinazojitokeza katika utatuzi wa migogoro ya Vyama vya Ushirika nchini kwa kuzingatia Sheria husika. Aidha, mwongozo huu ni nyenzo muhimu katika kutoa uelewa kwa walengwa na wadau mbalimbali kuhusu taratibu za utatuzi wa migogoro katika Vyama vya Ushirika kwa kuzingatia matakwa ya Sheria, Kanuni na taratibu za utatuzi wa migogoro. Hivyo, wadau wote wanaofanya kazi na Vyama vya Ushirika wanatakiwa kuhakikisha kuwa wanazingatia Mwongozo huu katika utatuzi wa Migogoro mbalimbali inayojitokeza kwenye Vyama vya Ushirika.



Dkt. Benson O. Ndiege
MRAJIS WA VYAMA VYA USHIRIKA

YALIYOMO

DIBAJI 2
SEHEMU YA KWANZA 4
UTANGULIZI 4
Migogoro 4
Mamlaka ya Kuandaa Mwongozo 4
Lengo na Madhumuni ya Mwongozo 4
Lengo kuu 4
Madhumuni 4
Wasimamizi (Ofisi ya Mrajis wa Vyama vya Ushirika) 4
Vyama vya Ushirika 5
Wadau 5
Walengwa wa Mwongozo 5
SEHEMU YA PILI 7
DHANA, AINA NA VYANZO VYA MIGOGORO KATIKA VYAMA VYA USHIRIKA 7
Dhana ya Migogoro na Viashiria vyake 7
Vyanzo vya Migogoro 7
Aina za Migogoro. 7
Athari za Migogoro 8
SEHEMU YA TATU 9
3.0 UTATUZI WA MIGOGORO KATIKA VYAMA VYA USHIRIKA 9
Taratibu za Utatuzi wa Migogoro 9
Ngazi ya Chama cha Ushirika 9
Ngazi ya Halmashauri 10
Ngazi ya Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa 10
Ngazi ya Mrajis 11
Ngazi ya Wizara 11
Mambo Muhimu ya kuzingatia 11
Mamlaka ya kutatua migogoro katika Vyama Vya Ushirika 12
Muda wa kushughulikia migogoro 12
Uzingatiaji wa Sheria na Kanuni husika 12
Uwazi na uzingatiaji wa haki za pande zote katika Mgogoro 13
Miiko na mipaka ya kushughulikia migogoro katika Vyama vya Ushirika 13
SEHEMU YA NNE 14
4.0 HITIMISHO 14

SEHEMU YA KWANZA

UTANGULIZI

Migogoro

Kwa mujibu wa Mwongozo huu, 'Mgogoro' ni mgongano unaotokea baina ya watu baada ya kutofautiana mawazo, mitazamo, uwajibikaji pamoja na mambo mengine yanayoweza kusababisha kutokuelewana baina ya pande mbili au zaidi kuhusu jambo fulani linaloweza kuleta madhara ya utendaji kazi katika Chama cha Ushirika.

Migogoro imekuwa chanzo kikubwa cha urudishaji nyuma wa maendeleo kwenye Vyama vya Ushirika kutokana na Vyama kutumia muda na rasilimali nyingi katika kusuluhisha Migogoro. Aidha, Viongozi, Watendaji na Wanachama kutokuzingatia Sheria, Kanuni na taratibu zinazotumika katika kusimamia uendeshaji wa Vyama vya Ushirika ndiyo chanzo kikuu cha Migogoro kwenye Vyama vya Ushirika.

Uwepo wa migogoro sio changamoto kwa Vyama vya Ushirika tu, bali pia kwa Serikali, katika kutimiza jukumu lake la kuvisimamia na kuhakikisha kuwa vinawahudumia wanachama wake kwa kuwapa huduma bora na zenye ufanisi kwa mujibu wa madhumuni ya kuanzishwa kwa Vyama hivyo. Hali hiyo imeifanya Serikali, kupitia Tume ya maendeleo ya Ushirika, kutumia muda na rasilismali nyingi katika kutatua migogoro ya Vyama vya Ushirika. Hivyo, kupitia mwongozo huu, Tume ya Maendeleo ya Ushirika itawezesha Maafisa Ushirika, Viongozi, Wanachama, Watendaji pamoja na Wadau wengine wa Ushirika kufahamu vyanzo mbalimbali vya migogoro pamoja na njia na taratibu mbalimbali za kutatua migogoro inayojitokeza kwenye Vyama vya Ushirika.

Mamlaka ya Kuandaa Mwongozo

Mwongozo huu umeandaliwa na kutolewa na Mrajis wa Vyama Vya Ushirika kwa kuzingatia Kanuni ya 81 ya Kanuni za Vyama vya Ushirika za Mwaka 2015.

Lengo na Madhumuni ya Mwongozo

Lengo kuu

Lengo la Mwongozo huu ni kuweka utaratibu utakaowezesha utatuzi wa migogoro ya Vyama vya Ushirika kwa ufanisi kwa kuzingatia matakwa ya Sheria, Kanuni na taratibu za uendeshaji na usimamizi wa Vyama vya Ushirika.

Madhumuni

Madhumuni ya mwongozo huu kwa wadau mbalimbali ni kama ifuatavyo:

Wasimamizi (Ofisi ya Mrajis wa Vyama vya Ushirika)

(i) Utawaongoza Maafisa katika kuzingatia taratibu za utatuzi wa Migogoro kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za Vyama vya Ushirika;
(ii) Utaongeza usimamizi kwenye Vyama vya Ushirika katika kuzuia uwezekano wa kutokea migogoro kwa kuhakikisha kuwa Vyama vya Ushirika vinatimiza wajibu wao

katika utekelezaji wa majukumu yao kwa mujibu wa Sheria,Kanuni na Masharti ya Vyama vyao;

(iii) Kuwa na ufahamu kuhusu hatua mbalimbali za utatuzi wa Migogoro;

(iv) Kuwa na ufahamu kuhusu mbinu mbalimbali za utatuzi wa Migogoro; na

(v) Kuelewa Vyanzo mbalimbali vya Migogoro na kuweza kuzuia Migogoro hiyo isitokee kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Vyama vya Ushirika.

Vyama vya Ushirika

(i) Utawezesha Wanachama, Viongozi na Watendaji kufahamu viashiria na Vyanzo vya Migogoro kwenye Vyama vya Ushirika;

(ii) Kuelewa nafasi ya kila mmoja katika kuzuia migogoro isitokee na kuchangia katika utatuzi wa Migogoro; na

(iii) Kuwezesha Wanachama, Viongozi na Watendaji kwenye Vyama vya Ushirika kufahamu utaratibu wa utatuzi wa Migogoro katika Ngazi ya Vyama vyao na kufahamu ngazi mbalimbali za utatuzi.

Wadau

Kuelewa nafasi na mipaka yao katika kushirikiana na Vyama vya Ushirika hasa katika utatuzi wa migogoro.

Aidha, pamoja na madhumuni kwa kila mdau yafuatayo ni madhumuni ya jumla ya Mwongozo huu: -

(i) Kuwawezesha Maafisa Ushirika, Warajis Wasaidizi na viongozi wa Vyama Vya Ushirika kushughulikia migogoro katika Vyama vya Ushirika kwa kuzingatia matakwa ya Sheria, Kanuni na Taratibu za Ushirika na Sheria nyingine za Nchi;

(ii) Kujenga uwezo kwa walengwa na wadau mbalimbali kufahamu taratibu za kisheria na kiushirika za utatuzi wa migogoro katika Vyama vya Ushirika; na

(iii) Kuwezesha migogoro ya Vyama vya Ushirika kutambulika, kushughulikiwa, kutatuliwa na kuratibiwa kwa wakati, kwa ufanisi na kwa kuzingatia Sheria na Kanuni husika.

Hivyo, Mwongozo huu ni muhimu kwa kuwa utasaidia kuwawezesha walengwa kujua taratibu za utatuzi wa migogoro katika Vyama vya Ushirika na matakwa ya Sheria, Kanuni na taratibu za Ushirika na Sheria nyingine husika zinazohusu utatuzi wa migogoro mbalimbali. Mwongozo huu utasaidia pia kuimarisha usimamizi wa Vyama vya Ushirika hususan katika udhibiti wa Migororo na athari zake kwa Vyama vya Ushirika na sekta ya ushirika kwa ujumla.

Walengwa wa Mwongozo

Mwongozo umeandaliwa kwa ajili ya kutumiwa na wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na:

(i) Maafisa Ushirika;

(ii) Wanachama, Viongozi na Watendaji wa Vyama vya Ushirika;

(iii) Watendaji na viongozi wa Wizara za Kisekta, Mamlaka za Serikali, na taasisi mbalimbali za umma zinazofanya kazi na Vyama vya Ushirika; na

(iv) Wadau wengine wa maendeleo

SEHEMU YA PILI

DHANA, AINA NA VYANZO VYA MIGOGORO KATIKA VYAMA VYA USHIRIKA

Dhana ya Migogoro na Viashiria vyake

Katika jamii migogoro ni jambo la kiasili kutokana na familia zetu kutoka katika jamii tofauti tofauti zenye tabia, mitizamo na tamaduni zisizofanana.

Migogoro huonesha kunyimwa au kudhulumiwa hadhi au hitaji fulani kwa mujibu wa makubaliano ya uanzishwaji wa Chama cha Ushirika. Ni matarajio ya kila mwanachama anayejiunga kwenye Chama cha Ushirika kuwa atapata huduma zinazostahili kwa viwango vinavyo kusudiwa kulingana na madhumuni ya uanzishwaji wa Chama chao, hivyo pindi huduma hizo zinapo kosekana au kupatika kwa viwango duni migogoro hutokea.

Vyanzo vya Migogoro

Migogoro mingi ndani ya Vyama vya Ushirika inatokana na Vyama kushindwa kuzingatia Sheria, Kanuni, taratibu na miongozo mbalimbali inayotumika katika kusimamia uendeshaji wa shughuli za hivyo. Miongoni mwa vyanzo vya migogoro ni pamoja na: -

i. Viongozi, wanachama na watendaji wa Vyama kushindwa kutimiza wajibu wao;
ii. Kutokuzingatiwa kwa taratibu za uingiwaji wa mikataba;
iii. kutorejesha mikopo kwa wakati katika Taasisi za fedha ambazo zinazo vikopesha Vyama vya Ushirika;
iv. Ubadhirifu wa mali za Chama;
v. Maafisa Ushirika kutosimamia Vyama ipasavyo;
vi. Huduma duni zinazotolewa na baadhi ya Vyama vya Ushirika;
vii. Ukosefu wa Elimu kwa Wanachama, Viongozi na Watendaji; na
viii. Muingiliano wa majukumu katika utekelezaji wa shughuli za Vyama vya Ushirika.

Aina za Migogoro.

Kumekuwa na migogoro mbalimbali inayojitokeza katika Vyama vya Ushirika ambayo ina athiri utendaji, uendeshaji na usimamizi wa Vyama vya Ushirika.

Kutokana na uzoefu, Migogoro inayojitokeza katika Vyama vya Ushirika mara kwa mara ni kama ifuatavyo: -

i. Mgogoro kati ya Mwanachama na Mwanachama mwingine;
ii. Mgogoro kati ya Chama cha Ushirika na Mwanachama;
iii. Mgogoro kati ya Chama cha Ushirika na Chama cha Ushirika kingine;
iv. Mgogoro kati ya Bodi ya Chama cha Ushirika, Watendaji na Mwanachama;
v. Mgogoro kati ya Chama cha Ushirika na wadau wengine wa Ushirika; na
vi. Mgogoro kati ya Chama na Afisa/Mamlaka inayosimamia Chama cha Ushirika.

Athari za Migogoro

i. Chama cha Ushirika kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria na hatimaye kuwa sinzia na kufikia hatua ya kufutwa kwa Chama na kufilisiwa;
ii. Kuyumba kwa biashara na kupelekea kupunguza mapato ya Chama;
iii. Taswira mbaya ya ushirika inayochangia kupungua kwa kasi ya watu kujiunga na Chama cha Ushirika pamoja na kupungua kwa idadi ya wanachama itapelekea Chama kufutwa na hatimaye kufilisiwa;
iv. Kupotea kwa rasilimali mbalimbali za Chama ikiwemo muda pamoja na mali za Chama itapelekea Chama kufutwa na hatimaye kufilisiwa; na
v. Kupoteza mahusiano kati ya Chama na wadau mbalimbali.

SEHEMU YA TATU

3.0 UTATUZI WA MIGOGORO KATIKA VYAMA VYA USHIRIKA

Kanuni ya 83 ya Kanuni za Vyama vya Ushirika za mwaka 2015 inatoa utaratibu wa kushughulikia Migogoro mbalimbali inayojitokeza kwenye Vyama vya ushirika. Mgogoro wowote kwenye Chama cha Ushirika utasuluhishwa kwa njia ya mazungumzo, majadiliano na makubaliano.

Hata hivyo, pamoja na uwepo wa kanuni hiyo, pamekuwa na changamoto katika ushughulikiaji wa migogoro hiyo. Hivyo, Mwongozo huu umeelekeza mifumo ambayo itasaidia utatuzi wa migogoro kwa ufanisi.
Mifumo hii itaweka utaratibu sahihi katika utatuzi wa Migogoro mbalimbali yanayojitokeza wakati wa utekelezaji wa majukumu kwenye Vyama vya Ushirika nchini kuanzia ngazi ya Chama hadi ngazi ya Wizara yenye dhamana na Ushirika.

Taratibu za Utatuzi wa Migogoro

Katika kushughulikia Migogoro ni muhimu kuwa na kumbukumbu ya Migogoro inayojitokeza na hivyo kuwa na umuhimu wa kuandikisha migogoro inayojitokeza ndani ya Chama cha Ushirika

Hivyo daftari/rejista inapaswa kuwepo katika ngazi zifuatazo:-

Ngazi ya Chama cha Ushirika

Ni wajibu wa Bodi ya chama kutatua migogoro yote chamani, na kuwa na daftari la kupokelea migogoro itakayojitokeza ndani ya chama chao. Daftari hilo litaonesha tarehe ya kupokelewa mgogoro, jina la muwasilishaji na mlalamikiwa katika mgogoro, maelezo ya mgogoro, na hatua za usuluhishi.

Mgogoro ndani ya Chama cha Ushirika utatatuliwa kwa kuanza na mazungumzo baina ya pande zinazohusika. Bodi itawajibika kwa migogoro yote inayojitokeza ndani ya Chama.

Bodi itapaswa kuunda kamati ya usuluhishi ambayo itashughulikia migogoro yote itakayojitokeza ndani ya Chama, ambayo itakuwa na wajumbe wasiopungua watatu (3) akiwemo mjumbe mmoja wa bodi, (wajumbe hao hawapaswi kuwa miongoni mwa wahusika katika mgogoro huo); na wajumbe wengine wawili (2) watatoka Miongoni mwa wanachama.

Kamati hii si ya kudumu, itaundwa pale tu mgogoro unapojitokeza, na itaundwa kulingana na aina ya mgogoro. Kamati hii itakuwa huru na itatakiwa kufanya maamuzi bila kushinikizwa wala upendeleo wowote; aidha, itawajibika kwa Bodi ya Chama. Endapo mgogoro utahusisha wajumbe wa Bodi, usuluhishi utapaswa kuhusisha Afisa Ushirika katika ngazi ya Halmashauri husika.

Mgogoro ndani ya Chama utashughulikiwa ndani ya muda usiozidi siku saba (7) tangu tarehe ya Mgogoro huo kupokelewa Chamani. Ikiwa Kamati itashindwa kusuluhisha mgogoro huo, itapaswa kumhusisha Afisa Ushirika katika ngazi ya Halmashauri.

Ngazi ya Halmashauri

Katika ngazi ya Halmashauri, Afisa Ushirika atapaswa kuwa na daftari la kurekodi migogoro yote itakayowasilishwa kwake na kufanya marejeo ya utatuzi katika ngazi ya Chama. Daftari hilo litapaswa kuonesha tarehe ya kupokelewa mgogoro huo, maelezo, hatua za usuluhishi na wahusika wa pande zitakazohusika na mgogoro huo na maoni ya Afisa Ushirika.

Baada ya marejeo hayo, Afisa Ushirika au Afisa aliyeidhinishwa atapaswa kushirikiana na kamati ya usuluhishi ya chama katika kusuluhisha mgogoro husika; na ikitokea kwamba kamati hiyo imeshindwa kumuwezesha Afisa Ushirika kutatua mgogoro huo, Afisa huyo ataweza kuutatua mgogoro huo yeye mwenyewe.

Mgogoro katika ngazi ya Halmashauri utashughulikiwa ndani ya muda usiozidi siku saba (7) tangu tarehe ya mgogoro huo kupokelewa.

Ikiwa Afisa Ushirika atashindwa kuusuluhisha mgogoro huo, atapaswa kuuwasilisha mgogoro huo kwa Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa au Afisa yeyote aliyeidhinishwa, kwa hatua zaidi.

Afisa Ushirika atapaswa kuwasilisha kwa Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa taarifa za migogoro yote iliyopokelewa na kushughulikiwa kwa kila kipindi cha miezi mitatu (3) au pale itakapoelekezwa na mamlaka yoyote. Vilevile, kama Afisa Ushirika atakuwa, kwa namna yoyote, anahusika na mgogoro unaosuluhishwa, hatatakiwa kushiriki katika kutatua mgogoro huo na badala yake mgogoro huo utapelekwa kwa Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa.

Ngazi ya Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa

Mrajis Msaidizi atapaswa kuwa na Rejista ya kusajili migogoro yote itakayowasilishwa kwake na kufanya marejeo ya utatuzi katika ngazi ya mamlaka husika. Rejista hiyo itapaswa kuonesha tarehe, maelezo, wahusika, hatua za usuluhishi, maoni na mapendekezo ya Afisa Ushirika/ Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa.

Baada ya marejeo hayo, Mrajis Msaidizi; atakavyoona inafaa; kwa kushirikiana na Afisa Ushirika katika kutatua mgogoro husika, anaweza kumshirikisha Afisa Ushirika katika ngazi ya Halmashauri. Endapo, kwa namna yoyote ile, Afisa Ushirika ataonekana kuhusika na Mgogoro huo, Mrajis Msaidizi atatatua Mgogoro huo yeye mwenyewe au atamhusisha Afisa Ushirika mwingine.

Mgogoro katika ngazi ya Mkoa utashughulikiwa ndani ya muda usiozidi siku kumi na nne (14) tangu mgogoro huo kusajiliwa kwenye Rejista ya migogoro ya Mkoa.

Ikiwa, mgogoro utashindwa kusuluhishwa katika ngazi ya Chama, Wilaya na Mkoa, mgogoro utawasilisha kwa Mrajis wa Vyama vya Ushirika kwa mujibu wa Kanuni ya 83(2) ya Kanuni za Vyama vya Ushirika za mwaka 2015. Uamuzi wa kuwasilisha mgogoro kwa Mrajis unaweza ukafanywa kwa azimio maalum la Mkutano mkuu, Bodi ya Chama, au mtu yeyote anayehusika kwenye mgogoro huo au Mwanachama wa Chama cha Ushirika husika.

Mrajis Msaidizi wa Mkoa atapaswa kuwasilisha kwa Mrajis taarifa za migogoro yote iliyopokelewa na kusajiliwa kwenye Rejista ya migogoro kila mwezi.

Ngazi ya Mrajis

Katika ngazi hii, pande zote zinazohusika na Mgogoro zinawajibika kufanya yafuatayo:

a) Mlalamikaji atapaswa kujumuisha nakala ya fomu ya usuluhishi ya ziada kwa ajili ya kumtumia Mlalamikiwa. Aidha, mara baada ya Mrajis kupokea fomu ya usuluhishi atafanya yafuatayo:-
   (i) Kusajili Mgogoro huo katika rejista ya Migogoro ya Vyama vya Ushirika ndipo hatua za utatuzi zianze; na
   (ii) Kugonga muhuri na tarehe ya kupokelewa Mgogoro na kutuma nakala yake kwa mlalamikiwa na wahusika wengine wa Mgogoro ambao kwa maoni yake wanaweza kuwa na maslahi katika mgogoro huo.

b) Mlalamikiwa kuwasilisha maelezo ya kujibu malalamiko yaliyo wasilishwa kuhusu mgogoro kwa Mrajis wa Vyama vya Ushirika ndani ya siku kumi na tano (15) tokea tarehe ya kupokea marejeo hayo kutoka kwa Mrajis.

c) Mrajis anaweza kutumia mamlaka aliyo nayo kisheria kuamua mgogoro huo yeye mwenyewe au kupeleka kwa msuluhishi (*abitrator*). Katika kutatua mgogoro huo, Mrajis ataweza kuteua kamati ya wataalam au watu wenye uelewa wa masuala ya ushirika na sheria kumsaidia kufikia uamuzi sahihi au ataweza kulipeleka jambo hilo kwa msuluhishi anayejitegemea baada ya kushauriana na pande zinazohusika katika mgogoro.

d) Ikiwa Mrajis, kwa mamlaka yake, ataamua mgogoro yeye mwenyewe atapaswa kushughulikia mapema iwezekanavyo kuuendesha usuluhishi wa mgogoro kama mashauri yanavyoendeshwa mahakamani; na ikiwa, kwa mujibu wa matakwa ya Kanuni za Vyama vya Ushirika, Mrajis ataamua kupeleka mgogoro kwa msuluhishi anayejitegemea, uendeshaji wa shauri la usuluhushi utakuwa kwa mujibu wa sheria ya usuluhushi (Abritration Act)

Ngazi ya Wizara

Upande usioridhishwa na uamuzi wa Mrajis katika mgogoro husika unaweza kukata rufaa kwa Waziri wa mwenye dhamana ya Ushirika. Katika rufaa ya mgogoro kwa Waziri mwenye dhamana ya Ushirika, uamuzi wa Waziri utakuwa wa mwisho.

Mambo Muhimu ya kuzingatia

Kwa lengo la kuhakikisha kwamba migogoro ya Vyama vya Ushirika inatatuliwa kwa wakati, ufanisi na kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu husika, mambo yafutayo yanapaswa kuzingatiwa kabla na wakati wa utatuzi wa migogoro:-

i. Mamlaka ya kutatua migogoro katika Vyama Vya Ushirika;
ii. Muda wa kushughulikia migogoro;
iii. uzingatiaji wa Sheria na Kanuni husika;

iv. Uwazi na uzingatiaji wa haki za pande husika; na
v. Miiko na mipaka ya kushughulikia migogoro katika Vyama Vya Ushirika.

Taarifa za Migogoro yote katika ngazi ya Halmashauri hadi Ofisi ya Mrajis wa Vyama vya ushirika itawasilishwa kupitia Mfumo wa Kielektoniki wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU) ambao migogoro itakayoanzia kwenye Chama itafuata hatua zote za kiutendaji kuanzia Ngazi ya Chama, Halmashauri, Mkoa mpaka kwa Mrajis bila kuruka hatua muhimu za utatuzi.

Mamlaka ya kutatua migogoro katika Vyama Vya Ushirika

Kwa mujibu wa Kanuni za Vyama vya Ushirika za Mwaka 2015, Mrajis wa Vyama vya Ushirika amepewa mamlaka na wajibu wa kutatua migogoro inayotokea katika Vyama Vya Ushirika. Aidha, Kanuni zimeelekeza utaratibu wa kuwasilisha migogoro hiyo na namna itakavyotatuliwa katika ngazi ya Chama cha Ushirika hadi ngazi ya Waziri mwenye dhamana na Vyama vya Ushirika.

Muda wa kushughulikia migogoro

Muda wa kushughulikia Migogoro katika ngazi mbalimbali utakuwa kama ifuatavyo:

(i) Katika ngazi ya Chama cha Ushirika, mgogoro utapaswa kushughulikiwa ndani ya siku 7 tangu tarehe ya Mgogoro huo kuwasilishwa na kupokelewa na Kamati husika, isipokuwa tu iwapo Masharti ya Chama yataelekeza vinginevyo;
(ii) Katika ngazi ya Wilaya/halmashauri, mgogoro utapaswa kushughulikiwa na Afisa Ushirika wa Wilaya/halmashauri ndani ya siku 7 tangu tarehe ya kupokelewa kwa mgogoro huo isipokuwa tu iwapo itaelekezwa vinginevyo; na
(iii) Katika ngazi ya Mkoa, mgogoro utapaswa kushughulikiwa na Mrajis Msaidizi ndani ya siku 14 tangu tarehe ya kupokelewa mgogoro huo isipokuwa tu iwapo itaelekezwa vinginevyo;

Katika ngazi ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika Makao Makuu, ambapo Mrajis anapokea rufaa, migogoro itakushughulikiwa na Mrajis ndani ya siku 30 tangu tarehe ya kupokelewa mgogoro huo.

Aidha, kwa migogoro inayohusu Mikataba, Makubaliano au Sheria zingine husika, migogoro hiyo itashughulikiwa ndani ya muda ulioainishwa katika Mikataba, Makubaliano au Sheria husika isipokuwa iwapo wahusika watakubaliana vinginevyo.

Uzingatiaji wa Sheria na Kanuni husika

Migogoro ya Vyama vya Ushirika inapaswa kushughulikiwa na kutatuliwa kwa kuzingatia Sheria zinazosimamia Vyama vya Ushirika na Sheria mbalimbali za nchi. Hivyo, kabla na wakati wa kushughulikia migogoro hiyo sheria zifuatazo zinapaswa kuzingatiwa:

(i) Sheria ya Vyama vya Ushirika (Sura ya 211), Kanuni za Vyama vya Ushirika na Masharti ya Chama kwa migogoro inayohusu masuala ya ushirika, hususan migogoro inayohusu wanachama na Viongozi au watendaji wa Vyama;

(ii) Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini (Sura ya 366), Kanuni zake na Kanuni za Utumishi za Chama kwa migogoro inayohusu masuala ya ajira na utumishi katika Vyama;
(iii) Sheria zinazosimamia masuala ya ardhi;
(iv) Sheria ya Usuluhishi; na
(v) Sheria zingine husika kwa migogoro inayohusu masuala mengine ikiwemo mikataba, manunuzi, uwekezaji n.k.

Uwazi na uzingatiaji wa haki za pande zote katika Mgogoro

Miongoni mwa mambo muhimu yanayopaswa kuzingatiwa wakati wa kushughulikia migogoro katika Vyama vya Ushirika ni pamoja na uwazi na uzingatiaji wa haki kwa pande zinazo husika. Taratibu zote za ushughulikiwaji wa migogoro ni lazima ziwe wazi kwa pande zinazo husika ikiwemo barua, taarifa, vielelezo na nyaraka zinazohusu mgogoro. Aidha, pande zote za mgogoro lazima zipewe haki ya kusikilizwa/kutoa maelezo ya ufafanuzi au utetezi ndani ya muda unaofaa (*reasonable time*) na uamuzi ufanyike kwa kuzingatia Sheria, kanuni na taratibu husika na bila upendeleo wowote. Ni lazima pia wahusika wafahamishwe haki yao ya kukata rufaa kwa mamlaka husika iwapo hawajaridhika na uamuzi uliotolewa.

Miiko na mipaka ya kushughulikia migogoro katika Vyama vya Ushirika

Pamoja na kuzingatia matakwa ya Sheria, Kanuni na taratibu za kushughulikia migogoro; mtu yeyote anayehusika na mwenye mamlaka ya kushughulikia mgogoro atapaswa kuzingatia miiko na makatazo yafauatayo:

(i) Kutokuwa na mgongano wa maslahi au sehemu ya mgogoro anaoshughulikia au kutuhumiwa na upande mmojawapo kuwa na maslahi na mgogoro huo;
(ii) Kutopendelea upande wowote wa mgogoro kati ya pande zinahosuhika na mgogoro husika;
(iii) Kutokupokea au kutoa rushwa kwa wahusika wa mgogoro au mtu yeyote mwenye maslahi na mgogoro huo;
(iv) Kutotumia lugha ya vitisho au isiyo na staha wakati wa kusikiliza maelezo ya pande husika za mgogoro; na
(v) kutofanya jambo au shughuli yoyote kinyume na Sheria ya Vyama vya ushirika na Sheria za nchi, Kanuni na taratibu za Ushirika.

SEHEMU YA NNE

4.0 HITIMISHO

Katika kuhakikisha kuwa kunakuwepo na Vyama vya Ushirika imara, endelevu na vyenye kukidhi mahitaji ya wanachama wake na jamii kwa ujumla, ni lazima kuwepo na uongozi thabiti, watendaji waadilifu na wanachama wanaoheshimu na kufuata Masharti ya Chama, Kanuni na Sheria ya Vyama vya Ushirika (Sura ya 211).

Aidha, Mwongozo huu unafuta Mwongozo wa utatuzi wa malalamiko na migogoro katika Vyama vya Ushirika Toleo la Mwaka 2022.